
Jarida la habari za kanisa jipya la kimitume afrika mashariki

Toleo la 2, Septemba 2011

# African Joy

*Toleo la bure*



• Kufanya maamuzi ya wazi

• Habari za kanda

## Ibada takatifu Mtume Mkuu huko Kigali

# Mtume Mkuu huko Kigali

Mwishoni mwa juma la tarehe 11 – 13 Februari 2011 Mtume Mkuu Leber alitembelea Rwanda, moja ya nchi nne za Afrika zilizo chini ya uangalizi wa Wilaya ya Kanada Kikanisa. Mitume kutoka nchi hizo nne waliweza kushiriki katika siku hizo za shangwe na pia waliutumia muda huo pamoja na Mtume wao wa Wilaya Woll aliyewekwa wakfu. Mtume Mkuu aliongoza Ibada mbili huko Rwanda: Moja huko Ruhengeri na nyingine huko Kigali, Mji Mkuu wa Rwanda. Baada ya ibada takatifu huko Kigali aliwasilisha hundi ya pesa Milioni 5 kwa Faranga za Kinyarwanda kwa Katibu Mkuu wa Mfuko wa Mauaji ya Kimbari.

Wapendwa wangu akina kaka na dada, nina furaha ya kuwa hapa na ni matarajio yangu kwamba moyo wa kila mmoja ujazwe baraka, furaha na amani. Katika maandiko Mtume Paulo anauliza swali la muhimu sana: "Ni nani atakayetutenganisha na upendo wa Kristo?" Awali ya yote ngoja niseme sisi wote tumeshuhudia upendo wa Kristo. Ametuleta nyumbani mwake, ametufanya kuwa wana wake na kutusamehe dhambi zetu. Upendo wake wa Kimungu ndio unaotubeba. Swali ni kwamba iwapo kuna jambo fulani linaloweza kututenga nisha na upendo huu.

Labda moyoni mwetu kuna mambo yanayoweza kututenganisha. Iwapo kuna mashaka na kutokuamini ndani ya mioyo yetu hili litatutenganisha na upendo wa Kristo kwa sababu pasipo imani hatuwezi kumpendeza Mungu. Jambo linalofuata: Iwapo moyoni mwetu tunapenda zaidi jambo fulani kuliko kumpenda Yesu Kristo. Hilo litatutenganisha naye. Mtafakari yule kijana tajiri aliyemwendea Yesu. Bwana alimwomba auze kila kitu na amfuate bali kijana huyu tajiri hakufanya hivyo. Kwa nini? Mali zake za kidunia zilikuwa muhimu zaidi kwake kuliko Yesu Kristo. Hilo lilimtenganisha na upendo wa Kristo.

Je kipi kingine kinaweza kututenganisha na upendo wa Kristo? Majivuno na kiburi! Msimamo huu umeelezwa katika kitabu cha Ufunuo: Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha wala sina haja ya kitu……. (Ufunuo 3:17). Tumeuona msimamo huo leo. Watu wengi wanadhani wanaweza kuishi pasipo Mungu. Wanadhani si lazima kumtegemea Mungu. Hilo linawatenganisha na upendo wa Kristo.

Jambo lingine linalotutenganisha na upendo huu ni kupungukiwa na kumtumaini Mungu. Ebu watafakari waliomwacha Bwana Yesu mara aliposema ni lazima wale mwili na kunywa damu Yake. Hawakulielewa hili na wakawa na imani haba. Walimwacha. Ebu na tujipime mioyo yetu. Ni hatari kunapokuwa na vishawishi vinavyotutenganisha sisi na upendo wa Mungu. Tunataka kufanya kama alivyofanya Mtume Paulo. Hatimaye alihitimisha kwamba hakuna jambo linaloweza kututenganisha na upendo wa Kristo: kukata tamaa, hakuna wazo lingine kuhusiana na maisha ya baadaye na hakuna ugomvi wala migogoro kwenye makusanyiko. Tunapenda kubaki waaminifu hadi mwisho.

Na Mungu atupatie neema ili kwamba sisi wote tuuelewe ujumbe huu na kutenda ipasavyo. (Imefupishwa)










*Mtume Mkuu na Mitume walitembelea Kumbukumbu ya Mauaji ya Kimbari mjini Kigali hapo aliweka shada la maua kwenye kaburi la pamoja na aliziombea nafsi zinazokadiriwa kufikia milioni 1 zilizopoteza maisha yao katika mauaji ya Kimbari yaliyofanyika huko Kigali mwaka 1994.*

*"Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?"*

*— Warumi 8:35*

# Kufanya maamuzi ya wazi

*Yesu alipata kusema kwamba ufalme ukigawanyika utaanguka.*



Historia inathibitisha hili. Ni falme na nchi ngapi ambazo hazikuanguka kwa sababu hakuna muafaka unaoweza kufikiwa katika mambo ya muhimu! Ndoa zimevunjika, familia zimetengana, na makampuni yaliyofanya biashara kwa muda mrefu yamefungwa kwa sababu watu hawakufikia makubaliano katika mambo ya muhimu.

Bwana anayafungamanisha mambo yafuatayo pamoja na mawazo yake maneno ya muhimu sana yanayowezekana: “Yeye asiyeambatana nami yu kinyume changu, na yeye asiyekusanya pamoja nami anatawanya”. Maelezo ya uwazi! Hii ina maana kwamba tunapaswa kufanya maamuzi ya uthabiti: ama kwa au dhidi ya Bwana. Hili ni jambo ambalo hatuwezi kuepuka. Wale wasiotaka kuamua kwa ajili ya Kristo, wale wasiomkiri Yeye kama Bwana na Mwokozi, wako kinyume naye bila kukwepa.

Watu wengi wanapenda zaidi kukwepa kufanya uamuzi wa uthabiti. Mara nyingi ni rahisi kuliko kuwa na msimamo wa wazi katika jambo fulani. Kama wapo katika nafasi mbili tofauti ya mambo wakati mwingine wanaamua juu ya jambo moja na pengine kwa upande mwingine yote yanategemea na kule wanakoona kuna manufaa kwao. Au watajaribu kuwa pande zote. Katika uhusiano wetu na Bwana hakuna uwezekano kama huo. Kwa vyo vyote haiwezekani tukawa pande zote mbele za Mungu. Inatakiwa kuwa upande mmojawapo. Kama hutaki kuamini kwamba mimi Ndiye utakufa katika dhambi zako. Ilimpasa Yesu awaambie watu wa rika lake. Wakati mwingine tunafanya maamuzi ambayo hatujajifunga kabisa, kwa sababu hatujashawishika kikamilifu. Hii inaweza kuonekana mapema au baadaye, kutoamua pale imani yetu inahusika kunaweza kutufanya mwishowe tuwe tunahoji kila kitu.

Hatuwezi kuwa pamoja na Bwana kwa asilimia mia hamsini na mahali fulani tena kuwa pamoja na asilimia hamsini. Pamoja na Bwana ina maana kwamba Yeye na Injili ndiyo kiini cha maisha yetu. Na tuipime mioyo yetu endapo tuna msimamo katika uamuzi wetu kwa Bwana na msimamo wetu katika kumkataa Shetani na kazi zake na njia zake. Hapa pia inatupasa kuamua kuwa upande mmoja.



*Mtume Mkuu Wilhelm Leber*





# africa Mashariki

## Kujenga Maisha Afrika Mashariki (KUMEA)

Kwa kufuatia wakati wa kuwekwa wakfu kwa Shadreck Lubasi kama Mtume wa Wilaya kwa Afrika ya Mashariki, alianza kutoa mapendekezo ya kuanzishwa kwa uwakala wa msaada wa ufadhili wa kanisa. Hatua hii ilikuwa ya lazima ili kukamilisha kutenganishwa kwa shughuli za kanisa na miradi ya misaada ya kibinadamu ambayo imekuwa ikiendelea kwa miaka mitano. Taasisi ya Henwood (Zambia) na NAK – Karitativ (Ujerumani) walitoa msaada wao kwa kusaidia kuanzisha shirika la msaada. Mnamo mwaka 2010, KUMEA ilikuwa imeanzishwa kikamilifu kabisa, Mtume Joseph Opemba Ekhuya kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa kwanza wa Shirika lisilokuwa la kiserikali.

Tangu hapo muundo umekwishawekwa kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi kwa kuwa na ofisi kamili – Sekeretarieti, inayoendesha kutoka South C, Nairobi na kamati za wenyeji zimeundwa kwa mikoa mbali mbali katika Kenya, KUMEA imeanzisha kamati za wenyeji (wanaojitolea) huko Machakos, Embu, Mwingi, Kisumu, Busia na Homabaty. Dira yake ni kuinua maendeleo ya shughuli za kiuchumi miongoni mwa wanajamii. Mpango unaotarajia kwamba Jamii salama inajitosheleza katika mahitaji yake iwe na usalama wa chakula na hufanya chaguo huru. Dhamana yake kuu ni kuendeleza uwezekano kwa watu kuboresha na kuitikia mahitaji ya Jamiii yao wenyewe. Dhamira hii imetokana na madhumuni yafuatayo.

- Kuchimba visima virefu na mabwawa ya maji.
- Kuajiri maafisa wa kilimo ili kuwafundisha watu mbinu za kilimo cha kisasa na kuwasaidia kupata ujuzi wa uongozi
- Kuinua, kukusanya na kutoa mifuko ya kipesa na rasilimali nyingine kwa ajili ya kuendeleza dira na dhamira ya shirika
- Kwa kuendelea na uanzishwaji wa kazi, KUMEA imechukua miradi ya maji na usafi iliyoanzishwa na kanisa katika Wilaya ya Mwingi. Pia KUMEA imeingia kwenye ushirikiano wa kibiashara na SUSTAINET-EA ili kusaidia kilimo asilia, NAKI – Kantativ (Ujerumani) na – Taasisi ya Henword (Zambia) wanatoa msaada wa kifedha na utaalamu. Zaidi sana shirika linaendelea kutafuta msaada wa kifedha na kitaalamu kutoka kwa watu wenye mapenzi mema na wanaojitolea.



***Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi akisaini Katiba ya mfumo wa huduma za KUMEA katika Afrika Mashariki.***



***Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi akiongoza sherehe za kufunguliwa kwa ofisi za KUMEA mjini Nairobi pamoja naye ni Mtume Opemba Ekhuya, Afisa Mtendaji Mkuu wa shirika.***



***Mtume wa Wilaya akiwa na wafanyakazi wa ofisi ya Utawala na Sekretarieti ya KUMEA, mara baada ya sherehe za ufunguzi wa KUMEA.***


# Kenya



Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi anakaribishwa na shada la maua kwenye kusanyiko la South C, Nairobi Kenya.







Mtume wa Wilaya akiongoza ibada takatifu kwa wilaya yote ya Nairobi kwenye kusanyiko la South C, ambalo ni kusanyiko kuu siku ya Jumapili tarehe 22 Mei, 2011. Wilaya ya Nairobi inajumuisha wilaya ndogo 6 chini ya Mtume Joseph Opemba Ekhuya.





Siku ya Jumamosi tarehe 21 Mei 2011 Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi alihudhuria tamasha la kwaya lililofanywa na Kwaya ya Wanafunzi Nairobi pamoja na kwaya ya watoto wa shule ya Jumapili.









Siku ya tarehe 21 Mei 2011 Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi alihudhuria tamasha la uimbaji, pamoja naye kutoka kushoto ni Maaskofu waalikwa: Sajembe (Mombasa), Askofu Ngugi (Embu), Askofu Kituo (Mombasa), Askofu Lukasi (Kirinyaga), Askofu Mwaniki (Nairobi), Askofu Nguli (Mwingi) na Askofu Mutinda (Nairobi). Kulia: Mtume wa Eneo Joseph Opemba Ekhuya na viongozi wa kiwilaya wakisikiliza kwaya.



Mtume Chrispin Kinyua na Mtume Likoko wakikaribishwa na watoto wa Shule ya Jumapili huko Taita, Taveta, Mombasa.



Mtume Peter Gitonga akikaribishwa na Vijana huko Karura – Kiambere.



Mtume Chrispin Kinyua na Mtume Ochieng wakikaribishwa na waumini huko Kilgoris (Eneo la kazi la Mtume Ochieng).



Mtume Jonathan Mutua akiwa na watumishi pamoja na waumini kabla ya kuanza kwa Ibada takatifu huko Nguni, Ngomeni (Eneo la kazi la Mtume Mutua).

# Uganda



*Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi akiwa na Mtume Kavuma akisalimia waumini mara baada ya Ibada takatifu huko Kacungiro, Uganda.*



*Kusanyiko la Makayi, Uganda wakati wa Ibada takatifu iliyoongozwa na Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi tarehe 18 Aprili 2011.*




*Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi akiwa na watumishi baada ya Ibada ya Jumapili ya Mitende kwenye kusanyiko kuu la Kampala.*



*Mtume Kimera pamoja na waumini baada ya kuzindua kanisa la Nyanga.  Baada ya Ibada takatifu Mtume alipanda mti.*





# Tanzania



*Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi akikaribishwa na kwaya huko Mwamukanga, Tanzania  Julai 2011, akiwa pamoja na Mitume na Maaskofu wenyeji.*




*Kusanyiko likiwa katika picha ya pamoja mara baada ya Ibada takatifu iliyoongozwa na Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi Julai 2011 huko Kijiji Kipya, nchini Tanzania.*



*Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi aliongoza Ibada takatifu  huko Dodoma, Tanzania.*



*Kusanyiko la Kamagambo Tanzania wakati wa Ibada takatifu iliyoongozwa na Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi.*



*Kwaya ikiimba kwa kumkaribisha Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi huko Gairo,  Tanzania.*



*Kusanyiko la Gairo Tanzania  kabla ya Ibada takatifu iliyoongozwa na Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi.*

# Wanakipaimara mwaka 2011, shughuli za watoto na vijana



*Mtume Peter Mutisya akiwa pamoja na wanakipaimara baada ya ibada ya kipaimara kwenye kusanyiko la Mnyanyani huko Kakuzi Kenya ya Kati.*




*Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi akiwa na watoto katika kusanyiko la Mwamukanga, Tanzania. Alifuatana na Mitume wenyeji wa eneo.*



*Kwaya ya watoto ikiimba kwa kumkaribisha Mtume Gitonga kwa Ibada Takatifu huko Karura, Kiambere.*



*Mzee wa Wilaya Edward Roberts na Mzee wa Wilaya Nyaga wakiwa pamoja na Wanakipaimara baada ya ibada ya kipaimara katika kusanyiko la Katina, huko Ngong.*




*Askofu James Mutinda akiwa pamoja na watoto baada ya ibada ya watoto katika kusanyiko la Mukuru, Nairobi.*



*Kwaya ya watoto ikiimba wakati wa Ibada Takatifu ya Kiwilaya iliyoongonzwa na Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi South C, Nairobi.*







*Mtume Kinyua akiwa pamoja na vijana huko Maua - Kenya Mashariki.*



*Mtume Mkuu akiwa pamoja na vijana mjini Kampala mwaka 2009, baada ya Ibada Takatifu.*



*Vijana wakimsindikiza Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi kwenye gari baada ya Ibada yenye furaha huko Dodoma, Tanzania.*



*Vijana wakicheza baada ya Ibada takatifu iliyoongozwa na Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi huko Karagwe, Tanzania.*

## Mtume Mpya na Askofu Mpya walipowekwa wakfu kwa ajili ya Wilaya ya Nairobi



**Mtume Joseph Opemba Ekhuya** alizaliwa katika familia ya Kimitume tarehe 1 Desemba 1969 akiwa ni mtoto wa kwanza kati ya familia ya watoto tisa (9). Kitaaluma ni msanifu wa majengo, ana shahada kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi. Kabla ya kujiunga na Shirika la KUMEA kama Afisa Mtendaji Mkuu amefanya kazi Kenya, Rwanda, Sheli Sheli na Msumbiji. Alimuoa Eddah Ositah Andrew tarehe 9 Machi 2002, na wamebarikiwa kupata watoto watatu (3). Alipata Madaraka ya ukuhani mwaka 1999, Mwinjilisti wa Jumuiya 2000 na Mzee wa Wilaya 2010. Wakati wa Ibada takatifu iliyoongozwa na Mtume Mkuu Wilhelm Leber mjini Kigali tarehe 13 Februari, 2011 Joseph Opemba Ekhuya aliwekwa wakfu katika utumishi wa utume. Eneo lake la kazi litakuwa Wilaya ya Nairobi lenye wilaya ndogo sita.



**Askofu James Kweta Mutinda** alizaliwa katika familia ya Kimitume tarehe 19 Novemba 1976 akiwa ni mzaliwa wa kwanza katika familia ya watoto 13. Yeye ni mwalimu kitaaluma, amekwishafanya kazi katika Sekta binafsi kwa miaka minane katika programu za kufundisha pamoja na Kamisheni ya Huduma za Walimu kwa miaka mitatu (3) kabla hajajiunga na Ofisi ya Utawala ya Kanisa kama Afisa Mkufunzi na Mawasiliano. Alimwoa Lucy Kitheka Septemba 2003, na wamebarikiwa kupata watoto watatu (3). Alipata madaraka ya Ushemasi mwaka 1997, Ukuhani 2000, Mwinjilisti wa Jumuiya 2004 na Mwinjilisti wa Wilaya 2006. Wakati wa Ibada ya Mtume Mkuu ya Februari 2011, James Mutinda aliwekwa wakfu kuwa Askofu. Eneo lake la kazi ni pamoja na wilaya ndogo tatu ; Embakasi, Kasaruni, na Kiambu zote zikiwa Nairobi.

# picha sanaa



*Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi alisherehekea pamoja na wanakwaya – kulia na chini baada ya tamasha la kwaya tarehe 21 Mei, 2011 huko South C, Nairobi, Kenya.*







*Mtume Kinyua na Mtume Ochieng wakipata mapokezi ya upendo toka kwa waumini baada ya ibada takatifu huko Kilgoris.*



*Mitume wakipumzika baada ya Ibada Takatifu iliyoongozwa na Mtume Mkuu Mjini Kampala, Uganda.*



*Mtume Peter Gitonga akijiunga na Kwaya inayoimba kwa furaha mara baada ya Ibada ya Pentekoste huko Mutungu.*


| | |
|---|---|
| **Limechapishwa na:** | **Kanisa Jipya la Kimitume Afrika Mashariki,** |
| **Tahariri:** | **Mtume wa Wilaya S. M. Lubasi,** |
| **Mhariri:** | **Kamati ya Uchapishaji ya Afrika Mashariki,** |
| **Mpangilio na Ubunifu:** | **Kundi la Kazi la Kimitume Wapya Afrika** |



**Ofisi ya Utawala: Anuani ya Posta 59041-00200, City – Square Nairobi, Kenya. Afrika Mashariki, Simu +254(20)6007701/6007702/6007706. Fax: +254(20)6000918, Barua pepe: admin@nac-ea.org**